


SHERIA ZA MAREKANI - HAKI NA MAJUKUMU

Inchini Marekani, sheria inalinda haki ya batu bote. Lazima ujifunze na kufuata sheria. Lazima ujue nini kinaweza kutokea ikiwa utavunja sheria.

Kwenda kinyume na sheria kunaweza kusababisha kulipishwa faini au kufungwa jela na kuharibu hali yako ya uwamiaji. Unaweza hata kufukuzwa mu inchi.



HAKI NNE ZA MSINGI ZA KUKUMBUKA:

1 Una haki ya kiraia, kama vile uhuru wa kusema na kujiunga na dini yoyote.



2 Una haki ya kufanya kazi. Hakuna mtu anayeweza kutumia rangi, dini, jinsia na asili ya kitaifa kukunyima kazi.



3 Batoto bote bako chini ya umri wa miaka 18 bana haki ya kuwa salama na kulindwa dhidi ya madhara.




4 Ikiwa wewe ni mhasiriwa wa uharifu, una haki ya kuchukuwa hatua ya kisheria. Ili kuripoti uharifu, ongeya na polisi. Ikiwa ni ya dharura, piga 911.




MAJUKUMU MANNE YA MUHIMU YA KUFUATA:

- 1 Ni kinyume cha sheria kumduru au kuumumiza mtu mwingine, wakiwemo watu wanafamilia. Madhara inahusu vitu kama, uonevu unyanyasaji, dhuluma/ya kijinsia, na unyanyasaji wa nyumbani.



- 2 Ni kinyume cha sheria kumlazimisha mtu kutenda kinyume na idhini yake hapendi. Hakuna mtu anayeweza kukulazimisha kuolewa au kukulazimisha kufanya kazi na usilipwe.



- 3 Ni kinyume cha sheria kuwanyanyasa watoto au kuwaacha watoto bila uangalizi wa mtu mzima .



- 4 Ni kinyume cha sheria kununua, kuuzisha au kutumia dawa ya kulevya fulani, kama vile heroini na kokeini.



SHERIA ZINGINE MBILI MUHIMU KUJUA:

- 1 Lazima uwe na umri wa miaka 21 ili uruhusiwe kununua au kunywa pombe.



- 2 Lazima uwe na lesensi ya dereva ili kuendesha gari.



Pia lazima ujifunze kuhusu sheria za serikali kuu na serikali za mitaa. Hii inajumuisha sheria zinazohusiana na uvutaji sigara katika maeneo ya umma, makazi, na uvuvi na uwindaji bila leseni.

Kumbuka: Kuna sheria nyingi nchini Marekani. Kutokujua sheria hakuzuii kuadhibiwa ukivunja sheria.

Cultural Orientation Resource Exchange

8719 Colesville Road, 3rd Floor • Silver Spring, MD 20910

For more information, visit the CORE Resettlement Navigator website at settlein.us.org.



The contents of this fact sheet were developed under an agreement financed by the Bureau of Population, Refugees, and Migration, United States Department of State, but do not necessarily represent the policy of that agency and should not assume endorsement by the Federal Government. **This material is in the public domain and may be reproduced.**